ukizingatia kuwa watu hao hawakuwa wamejiandaa kwa ajili ya jambo kama hilo bali niliwapigia tu simu na wengine wao bila hata kuwaonesha picha za eneo husika lakini jambo lililonishangaza walipokea mara moja na kukubali kuchangia fedha.

Baada ya kushirikisha watu **watano (5)** juu ya maono hayo na kukubali, huduma hii ilianza Mwezi **Januari** Mwaka **2021** tukiwa jumla watu **sita (6)** pamoja na mbeba maono*. Watu hao ni 1. Leonard Joseph 2. Upendo Munanga 3. Samwel Munanga 4. Furaha Kandore 5. Mr & Mrs Elias Mushi 6. Mimi na mke wangu Salome.*




*Picha ya pamoja ya waasisi wa huduma ya Tujenge Nyumba ya Mungu. Kutoka kulia ni Mrs. Mbogo (Salome), Mr. Mushi, Mr. Leonard, Mrs. Deo (Upendo), Mr. Mbogo, Mr. Samweli na Mr. Bonifasi. Kwenye picha hii anakosekama Mrs. Kipesee (Furaha Kandore) ambaye pia ni miongoni wa waasisi. (Picha terehe 12/03/2023).*

Niliunganisha watu hao watano kwenye kundi la **Whartsapp** ili kurahisisha mawasiliano na ukusanyaji wa michango ya ujenzi wa kanisa hilo la kijijini Kurusanga Wilaya ya Bunda Mkoani Mara. Watu hawa walijitolea kwa njia ya mali zao na hatimaye tukafanikisha ujenzi wa Kanisa hilo ndani ya kipindi cha miezi sita tu. Tulianza kuchangia ujenzi mwezi *Januari* na kukamilisha ujenzi mwezi *July, 2021*. Mara baada ya ujenzi huo kukamilika kwa ufanisi mkubwa, watu hao walivutiwa na huduma hiyo na hivyo baadhi yao walipendekeza kutovunjwa kwa kundi hilo la Whartsapp na badala yake iwe huduma